

JINA.....NAMBA YAKO..... TAREHE.....
SHULE..... SAHIHI YA MTAHINIWA.....

102/3
KISWAHILI
KARATASI YA TATU
FASIHI
Saa:2 ½

**MTIHANI WA TATHMINI-MUUNGO WA SHULE ZA
UPILI ZA
AINAMOI NA BELGUT 2010
JULAI / AGOSTI 2010**

102/3
KISWAHILI
KARATASI YA TATU
FASIHI
Saa:2 ½

MAAGIZO

- ❖ *Jibu maswali manne pekee.*
- ❖ *Swali la kwanza ni la lazima*
- ❖ *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki yaani;
Hadithi fupi, Riwaya ,Ushairi na Fasihi simulizi.*
- ❖ *Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.*

LAZIMA

1. Kifo Kisimani : Kithaka wa Mberia

“...Hakujua kwamba werevu mwingi huondoa maarifa. Alijiona pwagu. Lakini Butangi ina pwaguzi pia.”

- a) Haya ni maneno ya nani? (alama 1)
- b) Mnenaji anajirejelea kama pwaguzi kwa nini? (alama 4)
- c) Onyesha vile ambavyo hatima ya maneno haya yanamfanya mnenaji kuwa pwagu. (alama 5)
- d) Taja na ueleze pwaguzi wengine watano katika Butangi (alama 10)

HADITHI FUPI

MAYAI WAZIRI WA MARADHI: K.W. WAMITILA. JIBU SWALI LA 2 AU LA 3

MKIMBIZI: JOHN HABWE

- 2. (a) Eleza sifa za mkimbizi (alama 10)
- (b) Fafanua madhara kumi ya ukimbizi (alama 10)

MSAMARIA MWEMA: K.W WAMITILA

- 3. Aliendelea, “Unavyoona ni kama aligongwa...Basi mimi nilimkuta pale anagaragara chini”
 - a) Eleza muktadha wa kauli hii (alama 4)
 - b) Kuna usamaria wema unaoenda sambamba na isemavyo Biblia na kinyume chake katika hadithi hii. Eleza (alama 10)
 - c) “Mnyonge hana haki,” rejerea Likono kufafanua methali hii. (alama 6)

UTENGANO: SAID A. MOHAMED.

JIBU SWALI LA 4 AU LA 5

- 4. “...Kh, usiniseme Kizungu miye. Si ndivyo mlivyotuweka? Tuisome. Tuwe wajinga. Mtutawale na kutuparamia maisha, au sivyo?
 - a) Fafanua muktadha huu. (alama 4)
 - b) Ni vipi ambavyo mzungumzaji na wenzake wametawaliwa na kuparamiwa na wanaume? (alama 4)
 - c) Mzungumzaji na wenzake wamedhihirisha kuwa wana moyo wa ujasiri na wanaweza kumfanya chochote mwanamume. Thibitisha kwa mifano yoyote mitano. (alama 10)
- 5. Jadili risala ya mabadiliko katika riwaya ya utengano (alama 20)

SOMA SHAIRI LIFUATALO KISHA UJIBU MASWALI YANAYAFUATIA:

6. *Maneno musirukie*

Kurukia si kuzuri, maneno musirukie,
Mutakuja zusha shari, makonde muyabugie,
Mukimbie kwa ghururi, kama kuku mukimbie,
Maneno musirukie, wasemapo majabari.

Wasemapo majabari, maneno musirukie,
Hasa walio jeuri, kamwe musikurubie,
Ndoni zitawaaziri, na kwa Mola mutubie,
Maneno musirukie, wasemapo majabari.

Hii nayo ni kiburi, litemwalo murukie,
Yafaa mujihadhari, gumzo mulisikie,
Musije watu hasiri, magumi yawashukie,
Maneno musirukie, wasemapo majabari.

Imezukapo hatari, hii leo nikwambie,
Msemaji mhodari, uhodari ajitie,
Kapambana na jabari, la kufanya asijue,
Maneno musirukie, wasemapo majabari.

Kabla hayajakiri, jitu limgeukie,
Likamzaba hodari, naye mbio akimbie,
Likamkazia shari, na mbio asizijue,
Maneno musirukie, wasemapo majabari.

(Abedi K.A sheria za kutunga mashairi uk. 109)

- a) Onyesha mpangilio wa vina katika ubeti wa nne. (alama 2)
- b) Thibitisha matumizi ya pindu katika shairi hili (alama 2)
- c) Taja, ueleze na utoe mfano wa mbinu zozote mbili za uhuru wa ushairi zinazodhihirika katika shairi hili. (alama 4)
- d) Toa mifano miwili ya uradidi katika shairi. (alama 2)
- e) Kuna madhara gani kwa mtu anayerukia maneno? (alama 6)
- f) Fafanua dhamira ya mshairi (alama 4)

FASIHI SIMULIZI

7. (a) Eleza maana ya

(i) misimu

(ii) lakabu

(iii) ngomezi

(alama 6)

(b) Shauri mambo matatu anayopaswa kuzingatia mtu anapohitajika kufumbua fumbo

(alama 6)

(c) Fafanua umuhimu wa misemo

(alama 8)